
# Watu Wote Wanatakiwa Kufahamu Nini Kuhusu Maandiko.
# #4



Kwenye toleo la tatu tulijifunza kuhusu vipindi vitatu tofauti katika Biblia. Na tuliona leo sisi wanadamu tupo chini ya utawala wa Yesu Kristo tu. Pia tuliangalia kwa ufupi baadhi ya mambo tunayotakiwa kufanya kama tunataka kuwa ndani ya neno la Yesu.

Tukumbuke Mungu alitupa kila kitu tunachohitaji ili tupate uzima wa milele. Ni juu yetu siku hizi kuchunguza maandiko na kufanya kama ilivyoandikwa! Si kwa mapenzi yetu bali kwa mapenzi ya Mungu.


Kwenye toleo la nne, tutaangalia jinsi ya kuingia katika ufalme wa Yesu. Na jinsi ya kudumu humo. Tunaomba usiwe na moyo mgumu kama Farao. Na tukumbuke kama ni "Neno la Mungu; na ndivyo lilivyo kweli kweli," 1 Thes. 2:13.

Asante

Chuo Cha Biblia
S.L.P. 158
Chimala, Mbeya

Sehemu ya Kwanza


# Mungu Aliweka Maji Wapi?

| | |
|---|---|
| (1) **Nuhu**<br>Mwanzo 6:7-8<br>Ghalika |  Watu wanane waliokolewa kwa maji.<br>1 Petro 3:21. |
| (2) **Waisraeli**<br>Kutoka 14:26 |  Mungu aliokoa watu wake siku ile kwenye Bahari Nyekundu, Kutoka 14:30. |
| **(3)Waisraeli**<br>Yoshua 3 | Baada ya kutanga tanga kwa miaka 40, Mungu aliokoa Waisraeli kutoka jangwani kupitia Mto Yordani ili waingie kwenye nchi ya Ahadi. |
| **(4) Naamani Mwenye Ukoma** | Nabii wa Mungu alituma dawa ya uponyaji kwa mzee huyu, azame mara 7 kwenye mto Yordani. (2 Fal. 5) |
| (5) **Kipofu** | Alisafishwa kwenye kisiwa cha Siloam na akapona, Yohana 9.  |
| (6) **Nikodemo** | Yesu aliwaambia akizaliwa kwa maji na kwa roho ataweza kuingia katika ufalme wa Mungu, Yoh. 3:1-7. |
| (7) **Waumini** | Yesu aliwaambia wanafunzi wake wabatize watu ili waokolewa,<br>Marko 16:15-16. |
| (8) **Waumini** | Katika Mdo. 2:38, waliotubu na kubatizwa walipewa msamaha wa dhambi na kipawa cha Roho Mtakatifu. |

Kwa ufupi kama ni neno la Mungu, basi ndivyo lilivyo. Kama Mungu ameweka maji kwenye mpango wa wokovu, basi ndivyo ilivyo na sisi kama wanadamu hatuna mamlaka wala haki ya kubadirisha mpango wa Mungu.

---

**Sehemu Ya Pili**



**Ngazi Za Kwanza Katika Imani!**

1. Kutafuta wanafunzi!
2. Kuwabatiza wanafunzi!
3. Kuwafundisha kushika yote!

---

<u>Kabla ya kubatiza ni lazima kila mtu aamini!</u>

1. Bila imani hatuwezi kumpendeza Mungu, Ebr. 11:6.
2. Imani ni kuwa na hakika ya yale unayoamini, na kuwa na hakika kuhusu yale ambayo hatujayaona, Ebr. 11:1.
3. Chanzo cha imani ni kusikia na kujifunza neno la Mungu, Rum. 10:17.
4. Ngazi ya kwanza ielekee katika wokovu na kuamini kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, Yoh. 8:24.
5. Na imani hii inatuongoza ili tuzaliwe tena kwa maji na kwa roho, Yoh. 3:3-5; Mk. 6:16; Mdo. 2:38; 22:16.
6. Kama mtu atazaliwa tena, atakuwa kiumbe kipya na mshiriki wa Kanisa la Yesu, 2 Kor. 5:17; 1 Kor. 12:13; Efe. 1:22-23.
7. Na imani iliyomfanya mtu akubali injili ni lazima iongezeke, 2 Pet. 1:5-11; 1 Pet. 2:2.

## Mifano ya Imani

1. Habeli alionyesha imani kwa kuwa alikubaliana na mpango wa Mungu, hakufanya kama alivyotaka mwenyewe, Ebr. 11:4.
2. Henoko alitembea na Mungu kwa miaka 300. Kwa imani yake Alimpendeza Mungu, Ebr. 11:5; Mwa. 5:22.
3. Imani ya Ibrahimu ilimfanya aache nyumba yake na kufuata amri ya Mungu. Kwa imani yake alimfuata Mungu kila sehemu Mungu aliamua kuwaongoza Ibrahimu na familia yake. Pia kwa imani wakati imani yake ilijaribiwa, Ibrahimu alisimama kwenye upande wa Mungu, Ebr. 11:8-10; 17-19.
4. Wana Waisraeli walikuwa na imani walipomtii Mungu na kuzunguka mji wa Yeriko mara saba katika siku ya mwisho, Yos. 6:12-15, 16, 20; Ebr. 11:30. Baada ya kuzunguka mara saba kuta zilianguka na Waisraeli walivamia mji wa Yeriko ili wapewe nchi ya Ahadi.
5. Imani ni muhimu, ndio maana ni lazima tutunze imani zetu mpaka kufa, Ufu. 2:10; Mat. 10:22; 2 Tim. 4:6-8.

---

**Sehemu ya Tatu**

Marko 16:16, "Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini Atahukumiwa."

## Ubatizo wa Agano Jipya

Efe. 4:5—Kuna ubatizo mmoja!

## Sheria Tano Za Ubatizo

1. Ni lazima kuzamishwa (kuzikwa) katika maji, Rum. 6:4; Kol. 2:12.
2. Anaetaka kubatizwa ni lazima atubu, Mdo. 2:38; Mark 16:16.
3. Ni lazima akiri kuwa Yesu ni mwana wa Mungu, Mdo. 8:37; Rum. 10:10.
4. Ni lazima abatizwe kwa ajili ya ondoleo la dhambi, Mdo. 2:38; Mdo. 22:16.
5. Ni lazima abatizwe kwa mamlaka ya Mungu, Mat. 28:19.



Wewe utachagua nini?

**Mungu**…...Imani + Ubatizo = Wokovu, Mk. 16:16.
**Mwanadamu**…...Imani tu itakuokoa.

**Mungu**….Kutubu + Kubatizwa = Ondoleo la Dhambi, Mdo. 2:38.
**Mwanadamu**…...Kutubu bila kubatizwa ??

**Mungu**…...Tunazikwa katika Kristo, Rum. 6:3; Gal. 3:27.
**Mwanadamu**…...Kunyunyiza au kuruka bendera???

**Mungu**…...Ubatizo unasafisha dhambi zetu, Mdo.22:16.
**Mwanadamu**…..Ubatizo siyo muhimu, bora imani?????

**Mungu**…….Ubatizo unaokoa siku hizi, 1 Pet. 3:21.
**Mwanadamu**……..Wanadai ubatizo siyo lazima?????

---


Tufikiri kidogo????

Ni hekima ya nani leo inaokoa? Hekima ya Mungu au ya wanadamu, 1 Kor. 2:5. Jamani, mtoto hawezi kujua yaliyo mazuri, ni lazima mzazi amuonyeshe yaliyo mema. Mungu ni mzazi wetu leo, tukubali tu hekima yake.



---

Tukielewa ya kuwa, Mungu anahekima yote na anafahamu zaidi ya sisi ni nini kinachofaa kwa wokovu siku hizi, basi tutabarikiwa, Yer. 17:7. Lakini tusielewe tu, ni lazima tushike ukweli wa Mungu, Yak. 1:22. Na tukitunza na kuwa waaminifu kwake tutamwona mbinguni, Ufu. 2:10.



**Sehemu ya Nne**

Kupitia hekima ya Mungu alitupa kila kitu tunachohitaji na kutuongoza katika uzima wa milele.

---



Katika ulimwengu huu: Watu ni waovu, wamekufa kiroho. Wanatanguliza, ulevi, uongo, uvivu, wizi, ujinga, chuki, na aina ya dhambi nyingi sana, Rum. 3:23; 6:23.



Kwa kweli ulimwengu huu ni mali ya Shetani!

Lakini wote wanaoishi kama ulimwengu huu, na wote wanaoishi kwa mwili hawatauritihi ufalme wa Mungu mbinguni, Gal. 5:19-21.

---

Ili turithi mbinguni, Mungu (mwenye hekima yote) alitupa njia gani?

1. Ni lazima tusikie habari njema za Yesu Kristo, Mk. 12:29.
2. Ni lazima tuamini Yesu na kazi zake, Ebr. 11:6; Rum. 10:10.
3. Ni lazima tutubu, Lk. 13:3; 2 Kor. 7:10.
4. Ni lazima tukiri Yesu, Mat. 10:32; Rum. 10:9-10.
5. Ni lazima tubatizwe, Gal. 3:27; Rum. 6:3-4.

---

Tukifuata hekima ya Mungu, tutabatizwa ndani ya mauti yake:

1. Basi tumepatanishwa na Mungu, 2 Kor. 5:19.
2. Na tunaweza kupata uzima, ukoo ndani ya Yesu, 1 Yoh. 5:11.
3. Tutapata wokovu, Mk. 16:16; 2 Tim. 2:10.
4. Tutapata baraka za roho, Efe. 1:3.
5. Tutapata msamaha wa dhambi, Mdo. 2:38.
6. Tutasamehewa, Efe. 1:7.
7. Tutaingia ndani ya Kanisa, Ufalme Wake, 1 Kor. 12:13; Mdo. 2:47.

Baada ya hapo ni lazima tuishi maisha matakatifu mpaka tutakapokufa, na tutapewa taji, Ufu. 2:10.

# Sehemu Ya Tano

## Ni Lazima Uwe Ndani Ya Kanisa!

---

Kumbuka

Tunabatizwa kwa ondoleo la dhambi na baada ya kubatizwa; Mungu anatuongeza katika mwili wake, Rum. 6:3; Gal. 3:26-27; 1 Kor. 12:13. Na kama kichwa kisemavyo hapo juu ni lazima tuwe washiriki katika mwili (Kanisa) lake!

---

## Kwa nini ni lazima niwe mshiriki wa Kanisa?

### 1. Mungu anaongeza wote waliookolewa ndani ya Kanisa:

Mdo. 2:47 na Kol. 1:13.
Tumekwishaona katika toleo lililopita kwamba Kanisa ni Ufalme, kwa hiyo washiriki wa Kanisa tu wameokolewa kutoka gizani.

### 2. Kristo ni Mwokozi wa Kanisa:

Efe. 5:23; Kol. 1:18
Biblia haisemi Yesu ni Mwokozi wa kitu kingine!

### 3. Akatupatanisha na Mungu walio ndani ya Kanisa lake:

Efe. 2:16
Tunapatanishwa na Mungu kupitia mwili wa Yesu. Kama hatupo ndani ya Mwili yaani Kanisa, basi hatujapatanishwa na basi tutakuwa wa ulimwengu huu.

### 4. Kanisa ni Familia ya Mungu:

1 Tim. 3:15
Nyumba ya Mungu ni familia yake. Ni lazima watoto wa Mungu wawe ndani ya nyumba yake. Nyumba yake ni Kanisa, kama hujaingia katika familia ya Mungu basi ni lazima ubadirishe maisha yako.

### 5. Kwa sababu ni washiriki wa Kanisa tu waliopata bahati ya kuandikwa Mbinguni:

Ebr. 12:23; Ufu. 20:15.

## Sehemu ya Sita

## Mifano ya Waliookolewa Katika Agano Jipya!
## Mat. 28:18-20; Mk. 16:15-16.

| Mahubiri | Walio-amini | Wali-otubu | Waliokiri | Walio-batizwa | Matokeo |
|---|---|---|---|---|---|
| **Pentekoste** **Mdo. 2** | | Walitubu Mist. 37-38 | | Waliba-tizwa, 38-47 | Msamaha Wa Dhambi! |
| **Samaria** **Mdo. 8:5-13** | Waliamini Mst. 12 | | | Waliba-tizwa, 12-13 | |
| **Towashi** **Mdo. 8:35-39** | Aliamini, Mist. 36-37 | | Alikiri, 37 | Alibatizwa, 38 | Alifurahi, 39 |
| **Kornelio** **Mdo. 10:34-48** | Aliamini, Mst. 43 | | | Alibatizwa, 43-48 | Msamaha Wa Dhambi! |
| **Mlinzi** **Mdo. 16:31-32** | Aliamini, Mst. 31 | | | Alibatizwa, 33 | |
| **Lidia** **Mdo. 16:13** | Alishiriki, 14 | | | Alibatizwa, 15 | |
| **Kuhubiri Rum. 10:14** | **Kuamini Ebr. 11:6; 5:8-9.** | **Kutubu Luka 13:3** | **Kukiri Rum. 10:10** | **Kubatizwa Gal. 3:27** | **Wokovu 2 Tim. 2:10.** |
| **WEWE JE?** | | | | | |

Mwanafunzi,

Biblia ni wazi kuhusu kupata msamaha wa dhambi na jinsi ya kuingia katika Kanisa. Hakuna mahali kwenye Agano Jipya tunapoweza kuona mtu akibatizwa kwa kutumia maji madogo. Wote walizamishwa. Katika Yoh. 3:23, tunaona wakati Yohana Mbatizaji alikuwa anabatiza watu, alitafuta maji tele. Kwa hiyo ni lazima tufuate hekima ya Mungu! Pia kumbuka wale waliobatizwa siku ya Pentekoste, Mungu aliwaingiza wote katika Kanisa. Watu hawakupiga kula au kuandika barua ya maombi. Walibatizwa na Mungu aliwakubali!

Asante

## Maswali na Majibu
## (Sehemu ya Kwanza)

**Andika "N" kama sentence ni sahihi na andika "H" kama sentence siyo ya kweli.**

1. ________ Watu tisa waliokolewa katika safina.
2. ________ Yesu alimwambia Naamani ukibatizwa kwa maji na roho utakolewa.
3. ________ Chanzo cha Imani ni kusikia.
4. ________ Kama utaamini tu utakuwa kiumbe kipya.
5. ________ Henoko alitembea na Mungu kwa miaka 410.
6. ________ Waisraeli walizunguka mji wa Yeriko mara 6 katika siku ya saba, ili kuta zianguke.
7. ________ Kuna ubatizo wa aina nyingi.
8. ________ Ubatizo ni ishara tu kwa walioamini.
9. ________ Ubatizo ni kwa msamaha wa dhambi.
10. ________ Hekima ya wanadamu inafaa kupeleka mtu kwa Mungu.
11. ________ Petro ni mwokozi wa Kanisa.
12. ________ Kanisa siyo mwili wa Yesu.
13. ________ Ni lazima Kanisa likubaliane na kupiga kura kabla ya kuingiza mtu Kanisani.
14. ________ Towashi alikiri ya kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu.
15. ________ Yohana Mbatizaji alitafuta maji tele kabla ya kubatiza watu.

Rudisha Majibu Kwa:
C.S.O.P.
S.L.P. 158
Chimala, Mbeya

# Maswali na Majibu
# Sehemu ya Pili

1. Nani alikwenda kumwona Yesu ilifahamu zaidi kuhusu Ufalme wa Mungu?
   ___________________________________
2. Yesu alimwambia kipofu katika Yohana 9, asafishe macho yake wapi?
__________________
3. Kama mtu ataamua kubatizwa Mungu atamweka kwenye Kanisa la nani?
   ____________________________________
4. Kanisa ni familia ya ________________________.
5. Kufuatana na Efe. 1:3, kama sisi ni watoto wa Mungu tutapata nini?
   _____________________________

# Sehemu ya Tatu

**Chagua mstari sahihi unaothibitisha mawazo hapa chini, kati ya mistari yote.**
**Kila jibu itatumika mara moja tu.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mdo. 2:38 | Ebr. 11:6 | Mk. 16:16 | Ufu. 2:10 |
| 2 Kor. 5:19 | Efe. 5:23 | Yn. 3:1-7 | Yn. 8:24 |
| Mdo. 22:16 | 1 Pet. 3:20-21 | Rum. 3:23 | 1 Tim. 3:15 |
| Rum. 10:10 | Kol. 2:12 | 1 Kor. 2:5 | Yak. 1:22 |
| Efe. 1:3 | Gal. 5:19-21 | 2 Tim. 2:10 | 1 Yn. 5:11 |

1. Ubatizo kama safina unaokoa siku hizi, ______________________.
2. Tusifuate hekima ya wanadamu, _______________________.
3. Tuishi maisha matakatifu mpaka siku ya mwisho, ____________________.
4. Ubatizo unaosha dhambi zetu, _____________________.
5. Hatuwezi kumpendeza Mungu bila imani, _________________.
6. Watu wote ni wenye dhambi, ___________________.
7. Tusiwe wasikiaji tu, ____________________.
8. Ni lazima tumkiri Yesu Kristo, ____________________.
9. Matendo ya mwili yatafanya tusiingie mbinguni, _________________.
10. Ni lazima tubatizwe kwa maji na roho, __________________.
11. Tunaweza kupata uzima wa milele kupitia Yesu tu, _______________________.
12. Tubuni na kubatizwa mtaokoka, ___________________.
13. Ubatizo wa maandiko ni kuzikwa, ____________________.
14. Tukiamini na kubatizwa tutaokoka, ____________________.
15. Nyumba ya Mungu ni Kanisa lake, ____________________.
16. Yesu alitupatanisha, _______________________.
17. Kristo ni kichwa cha Kanisa, _______________________.
18. Wokovu unapatikana katika Kristo Yesu, ____________________.
19. Tusipoamini Yesu ni mwana wa Mungu tutakufa, _____________________.
20. Mungu ametubarikia sisi na baraka zote za rohoni, _____________________.

Toleo lijalo tutaangalia, jinsi Mungu anataka watoto wake waishi na jinsi ya kumuabudu Yeye.
Asante.

Jina la Mwanafunzi ________________________________
Anwani: ______________________________
______________________________.

Kama unataka tuwatumie watu wengine masomo haya kwa njia ya posta
Andika majina na anwani zao kisha tuma majina yao:

C.S.O.P.
S.L.P. 158
Chimala, Mbeya